

Wanafunzi wa shule ya Middle wanao furahia majaribio ya STEM wakati wa Mpango wa Masomo Majira ya Joto katika DelSesto Middle School.

# MIUNGANISHO

JULAI 20, 2023

## KONA YA AFISA MKUU MSIMAMIZI



**DKT. JAVIER MONTAÑEZ**
AFISA MKUU MSIMAMIZI

Katika Shule ya Wilaya ya Providence, Julai ni wakati ambao watu wengi wanachukua likizo ambazo wanahitaji kabisa, walimu wako likizo katika mapumziko ya majira ya joto, na wasimamizi wanafanya kazi kwa bidii kuhakikisha mpito mzuri hadi kwa mwaka mpya wa shule. Wakati huo huo, bado kuna mipango kabambe ya mafunzo ya majira ya joto yanayo tekelezwa katika vyuo vilivyo teuliwa.

Wiki iliyopita, nilifurahia kutembelea washirika wetu wa mipango iliyoendeshwa katika Bailey Elementary School kupitia **Meya Brett Smiley**. Tuliona wanafunzi wa Providence wakifurahia mpango mzuri ulio ongozwa kupitia **Inspiring Minds**, **Sylvan Learning** na **YMCA**. Wiki ijayo, nitatembelea mipango ya Wilaya pamoja na **Gavana Dan McKee** na **Kamishina wa RIDE Angélica Infante-Green**.

Nimefurahia kusoma kuhusu majaribio halisi yanayo fanyika katika mipango yetu ya middle school katika **DelSesto Middle School**. Wiki iliyopita, walijifunza jinsi bembea ya kuzunguka inafanya kazi kwa kutumia nishati ya uwezo, nishati ya kinetiki na nishati ya mekanika. Katika jengo hilo hilo, wanafunzi wengine walikuwa wanafurahia mpango wa mashindano ya E-Michezo.

Katika **Lima Elementary**, walimu wawili waliongoza masomo kulingana na kitabu cha *Kwa sababu ya Winn-Dixie* kilichoandikwa na Kate DiCamillo. Kupitia hadithi hii, wanafunzi wali chambua mada ya msamaha, kushiriki na tumaini. Shule zetu zika hai pamoja na mafunzo ya majira ya joto katika viwango vyote vya darasa. Mnamo Agosti 12, wanafunzi wa darasa la juu wanao shiriki katika mpango wa mafunzo kwa majira ya joto katika shule ya sekondari watapokea diploma zao za sekondari wakati wa sherehe ya kuhitimu katika **Akademia ya Taaluma na Ufundi ya Providence**! Jukwaa litakuwa upinde wa bendera za shule na rangi zinazo wakilisha kila shule ya sekondari.

Wakurugenzi wa mpango wa majira ya joto wamekuwa wakikaribisha wazazi katika shule kuona utekelezaji wa mpango na kujibu swali lolote. Wakurugenzi wameripoti kwamba imekuwa bora kuona wazazi wakijishughulisha kiamilifu katika uzoefu wa masomo ya mtoto.

Wakati wengi wenu wanatumia mapumziko haya kufurahia muda wao pamoja na familia na marafiki, nawa himiza kuchukua muda kusoma pamoja na watoto wako na kuchukua muda kusoma wewe mwenyewe. Tunafahamu kwamba wanafunzi hawawezi kufanya bidii wakiwa peke yao. Wanafunzi wako katika safari hii ya kielimu pamoja na watoa huduma wao upande wao. Ikiwa utachukua muda kujumuisha shughuli za kufurahia katika masomo katika siku, wanafunzi watavuna manufaa ya kielimu na kijamii. Lengo ni kuepuka kukosa mafunzo ya majira ya joto na kufanya wanafunzi wetu kuwa tayari kwa shule na kuwa na hamu kusoma.




## KUBORESHA VIFAA

Wafanyakazi na wakandarasi wa PPSD wanafanya kazi kwa bidii kuhakikisha wanafunzi wanapata majengo ya shule na madarasa yanayo mng'aro na kualika kwa mwaka mpya wa shule. Tuta fungua milango katika **D'Abate Elementary School**, **Spaziano Elementary School** na **Pleasant View Elementary School zilizo rekebishwa hivi majuzi katika Narducci Early Learning Center katika** majira haya ya vuli.

Milango ita funguliwa kirasmi katika ukumbi wa **Hope High School** baada ya matayarisho ya mwisho ya urekebishaji wake kamili wa milioni $ 20. Na **Classical High School** inaendelea na urekebishaji wake hatua kwa hatua ikiwa na upande mpya wa Hisabati ulio rekebishwa. Shukrani kwa timu yetu ya bidii ya **operesheni na uwezeshaji ya PPSD** na hata pia **Idara ya Elimu ya Rhode Island (RIDE)** timu ya Operesheni.

Tafadhali chukua muda kutazama marekebisho katika Kituo cha Narducci katika video hapo juu.

# TAARIFA MPYA ZA WILAYA

## KIZIRIAN IMETAMBULIKA KAMA NYOTA - 5 MPANGO WA KABLA YA CHEKECHEA

PPSD, pamoja na **Gavana Dan McKee** na **Idara ya Elimu ya Rhode Island (RIDE)**, wamefurahia kutangaza kwamba mpango wa **Harry Kizirian Elementary School Pre-Kindergarten (Pre-K)**ume tuza **BrightStars** alama ya nyota-5. Hii ndio alama yao ya juu zaidi. Wao ndio shule ya pili Wilayani kupokea alama ya nyota-5. BrightStarsina tathmini huduma za utunzaji wa watoto, shule za chekechea katika shule za umma, nyumba za huduma ya watoto kwa familia na mipango ya kipekee ya umri wa shule kati ya viwango kadhaa vya vipimo na vigezo vya ubora. Muungano wa Rhode Island kwa Elimu kwa Watoto Vijana ni wakala ya usimamizi wa BrightStars. Rhode Island AEYC ni mshiriki wa jimbo kwa Muungano wa Kitaifa kwa Elimu ya Watoto Vijana (NAEYC).

## NYAKATI ZA KENGELE KWA MWAKA WA SHULE 2023-2024

PPSD ili peana usasisho wa **Nyakati za Kengele** na **Kalenda ya Kielimu** kwa familia mwishoni wa Juni. Usasisho ulikuwa kwa sababu ya kura ya kuratibu makubaliano ya mwaka wa shule 2023-2024 kutoka kwa Muungano wa Walimu wa Providence (PTU). Kandarasi hii ya mwaka mmoja inapendekeza kutekeleza dakika 30 za ziada katika mafunzo kila siku, siku nne za maendeleo ya kitaaluma kwa mwaka wakati wa Agosti kwa walimu na dakika 90 baada ya kila wiki mbili wakati wa masaa ya nje ya shule. Kwa orodha iliyo sasishwa ya nyakati za kengele, tafadhali bofya hapa. Unaweza pata kalenda iliyo sasishwa ya masomo hapa.

## ONGEZEKO LA UFADHILI WA EQUITY

**Ufadhili wa Equity** unawezesha wanafunzi na walimu kujaribu mawazo mapya ya ubunifu na uvumbuzi unao saidia ufundishaji na masomo bora, na pia kuboresha uelewaji na kuthamini utamaduni, kujitolea kupinga ubaguzi wa rangi na kuelewa ushirikiano wa kijamii na demokrasia. Ongezeko la Ufadhili wa Equity utafadhili miradi katika bajeti kati ya $500 na $4900, kila mwaka.

**Nani anaweza kuwasilisha ombi?** Idara/Wafanyakazi wa PPSD kwa niaba ya darasa, shule, na/au kama mfadhili wa mradi ulio ongozwa na mwanafunzi, wanaweza kuwasilisha ombi.

**Siku ya mwisho ya usajili:** Maombi yana kubaliwa kama yanavyo wasili. Ikiwa unapendelea kufuatilia mradi tafadhali wasilisha hapa ombilako.



# USAWA NA USHIRIKI

## Usawa wa Mwanafunzi Akademia ya Uongozi wa Majira ya Joto

**Usawa wa Mwanafunzi Akademia ya Uongozi wa Majira ya Joto**, ulioandaliwa kupitia Ofisi ya Usawa na Ushiriki, ni idara ya wiki mbili iliyowekeza kuboresha ujuzi wa wanafunzi katika kuwaza kwa umakini, uongozi, ushauri, kusoma na kuandika. Mpango wetu umeundwa kuwezesha wasomi vijana wawe na vifaa na ufahamu unao hitajika kutengeneza mabadiliko muhimu katika jumuiya zao. Akademia hii itafanyika **Agosti tarehe 15, 2023** hadi **Agosti tarehe 25, 2023**. Washiriki watakutana katika Chuo kikuu cha Brown, katika Main Green, katika muda wa Akademia hiyo. Wageni waendeshaji walioalikwa wanajumuisha: **Austin Martin**, **A.R.I.S.E** na **Non-Violent Schools Rhode Island**.

## Timu ya Uongozi wa Usawa Mabalozi Viongozi:

Timu ya Uongozi wa usawa ni kikundi cha washika dau tofauti: walimu, wafanya kazi, wazazi, wanajumuiya, na wanafunzi wanao fanya kazi pamoja kupangua, kuchambua, na kuelewa masuala ya usawa, utofauti, ujumuishaji na ushirikishaji ambayo yanapatikana katika shule yao au wilayani. Timu za uongozi wa usawa unatetea mabadiliko na usaidizi kujenga uwezo kwa viongozi wa shule wenye kuzingatia usawa, wakati wanapo saidia kutengeneza mipango kuhusu jinsi ya kutekeleza na kudhibiti mabadiliko kwa ufanisi.

Bado tunaendelea kupokea maombi kutoka ndani ya nyumba. Tunatafuta walimu wawili katika kila shule kushiriki katika mafunzo haya ya uongozi ulioundwa kipekee, unao kusudiwa kutayarisha wote kuongoza timu za uongozi wa usawa katika shule zao wakati wa mwaka wa shule 2024-25. Mafunzo yatadumu mwaka mzima na yatafuatilia msingi wa mada unao jadiliwa katika *Mitindo Tano ya Uongozi Unaolenga Usawa*. Mafunzo yataendeshwa kupitia mmoja wa waandishi, **Dkt. Mark Gooden**. Kwa sababu ya usasisho wa hivi majuzi wa kalenda, tarehe mpya za mafunzo ya majira ya joto ni **Agosti 23 na 24 kuanzia 9am-2pm**, eneo litatangazwa. Ikiwa una pendelea kuwasilisha ombi tafadhali hakikisha kuongea na Mwalimu mkuu wako.

## Muhtasari wa Ripoti ya Habari Njema

Hii **Ripoti ya Idara ya Vipimo ya OEB** inapeana muhtasari kwa ufupi kuhusu utendaji na mafanikio yaliyo tekelezwa kupitia Ofisi ya Usawa na Ushiriki tangu uanzilishi wake upya mnamo Julai 2023. Inajumuisha vipimo vikuu na hatua muhimu zote zilizo tekelezwa na mipango ya siku zijazo. Hati hii ina hudumu kama uelewa kamili wa kila maendeleo ya idara na inasaidia kuhakikisha uwazi pamoja na washika dau muhimu na washiriki wa jumuiya ya PPSD.

## Toleo la Maendeleo ya Kitaaluma Yajayo

Ofisi ya Usawa na Ushiriki itapeana maendeleo ya kitaaluma na mafunzo mwaka mzima huu ujao, ikijumuisha **Wiki ya Maelekezo**. Ikiwa unapendelea kualika ofisi katika shule yako kuonyesha katika idara yako au wafanyakazi wakati wa Wiki ya Maelekezo (Agosti 28-31), tafadhali tia saini hapa.

# NI HABARI NJEMA: PPSD KWENYE VYOMBO VYA HABARI

- Mtoa huduma  kwa Providence school ana nia ya kuajiri wafanyakazi 200+ walio sitishwa ajira kupitia mtoa huduma wa awali
  *Jarida la Providence*, Julai 10, 2023
- Shule ya Providence middle school inatekeleza sera kuzuia matumizi ya simu ya rununu wakati ukiwa darasani
  *WJAR*, Julai 14, 2023

# KUWASHEREHEKEA WANAFUNZI

Wanafunzi wetu wenye bidii na wenye talanta wanafanya mambo mazuri kila siku. Hapa kuna mifano michache.





## IDADI YA UFADHILI WA MASOMO

Tulitaka kuangazia na kupeana hongera kubwa kwa **wanafunzi wetu wa darasa la juu wa PPSD** ambao wamehitimu tu mnamo Juni na walituzwa ufadhili wa masomo kuendelea na elimu yao. Hapa chini ni idadi ya ufadhili wa masomo katika kila shule ya sekondari huko PPSD. Ufadhili wa masomo unaotuzwa unajumuisha Msaada wa Serikali Kuu na Jimbo, Ruzuku za Nje, Ufadhili wa Kimataifa wa Masomo na zote zina fuatiliwa. Ufuatiliaji unajumuisha ufadhili wa masomo uliotuzwa kutoka kila idara ya juu ya masomo walipo sajiliwa, sio tu zile wanazo hudhuria. Hongera kwa wote!

| Shule za Sekondari | Dola za Ufadhili wa Masomo Zilizopokewa |
|---|---|
| 360 | $3,420,865.00 |
| Alvarez | $2,939,281.00 |
| Central | $5,663,851.00 |
| Classical | $18,320,000.00 |
| E-Cubed | $2,645,169.00 |
| Hope | $2,579,255.00 |
| JSEC | $704,350.00 |
| Mt. Pleasant | $4,410,150.00 |
| PCTA | $2,782,530.00 |
| Idadi | $43,465,530.00 |

## MIPANGO YA MAJIRA YA JOTO

**Mipango ya Majira ya Joto**yanatekelezwa kikamilifu, na wanafunzi wanasoma kupitia mtaala kabambe pamoja na walimu waliojitolea! Shukrani kubwa kwa walimu waliochukua muda wao nje ya majira yao ya joto kusaidia kusomesha wanafunzi wetu. Tazama picha kutoka Mipango kadhaa ya Masomo ya Majira ya Joto hapa kuona kile wanafunzi wetu wa PPSD wamekuwa wakifanya katika wiki kadhaa zilizo pita!

## WEKA ALAMA KWENYE KALENDA ZENU

- **SIKU YA USHINDI (HAKUNA MPANGO WA MAJIRA YA JOTO) JUMATATU, AGOSTI 14, 2023**
- **SIKU YA MWISHO YA MPANGO WA MASOMO YA MAJIRA YA JOTO ALHAMISI,** Agosti 17, 2023
- **SIKU ZA MAENDELEO YA KITAALUMA KWA MWALIMU JUMATATU, AGOSTI 28 - ALHAMISI, AGOSTI 31**
- **SIKU YA WAFANYAKAZI** (Hakuna Shule) Jumatatu, Septemba 4, 2023
- **MAELEKEZO KWA WALIMU** (Hakuna Shule kwa Wanafunzi) Jumanne, Septemba 5, 2023
- **SIKU YA KWANZA SHULENI** Jumatano, Septemba 6, 2023

Providence Schools

© 2023 Providence Public Schools · communications@ppsd.org · www.providenceschools.org

Mambo ya kusisimua yanatokea katika Wilaya nzima na tunataka kueneza ujumbe! Ikiwa una programu, hafla, Mfanyakazi au mwanafunzi mwenye hadithi nzuri ajabu ambayo ungependa kuonyesha, tafadhali tuma barua pepe kwa communications@ppsd.org.